


Ireland



An Roinn Dlí agus Cirt,
Gnóthai Baile agus Imirce
Department of Justice,
Home Affairs and Migration



UNACHOHITAJI KUJUA KUHUSU EURODAC



SWAHILI

➤ KWA NINI NAPOKEA KITABU HIKI CHA MAELEZO?

Unapokea brosha hii kwa sababu data yako ya kibayometriki inahitaji kuchukuliwa na mamlaka.



Data ya kibayometriki inamaanisha alama za vidole na picha yako.



Data hii, pamoja na taarifa kuhusu utambulisho wako na taarifa nyingine muhimu, itatumwa kwenye hifadhidata ya Eurodac.

Haki zako wakati wa mchakato huu na kile kinachotarajiwa kutoka kwako kimeelezwa katika brosha hii.

➤ EURODAC NI NINI?

Eurodac ni hifadhidata ya Ulaya inayohifadhi na kulinganisha taarifa kuhusu makundi fulani ya watu wanaoingia katika nchi za EU+. Makundi haya yameelezwa kwa undani katika brosha hii.

Hifadhidata hii inatumiwa na nchi 31 za EU+ ambazo zinaweza kuchakata data zako na kupata taarifa zako. Ukisafiri kwenda nchi nyingine ya EU+ bila ruhusa na data zako zikachukuliwa tena, data zako zote zilizohifadhiwa katika Eurodac zitaonwa na mamlaka ya nchi hiyo. Katika baadhi ya matukio, data zako zitasasishwa na taarifa mpya.

➤ NI NCHI ZIPI ZA UMOJA WA ULAYA EU+?

Sasa uko nchini Ireland ambayo ni mwanachama wa Umoja wa Ulaya [EU+].

Nch wanachama wa EU+ ni:



Nchi 27 wanachama wa Umoja wa Ulaya (EU): Austria, Ubelgiji, Bulgaria, Kroatia, Saiprasi Jamhuri ya Czech, Denmark, Estonia, Ufini, Ufaransa, Ujerumani, Ugiriki, Hungaria, Italia, Latvia, Lithuania, Luksemburgu, Malta, Uholanzi, Poland, Ureno, Jamhuri ya Ireland, Romania, Slovakia, Slovenia, Uhispania, Uswidi na



Nchi nyingine 4: Iceland, Liechtenstein, Norway na Uswisi.

➤ EURODAC INA LENGU GANI?

Eurodac ina malengo makuu matano:

- ✔ kusaidia nchi za EU+ kuamua ni nchi gani ina jukumu la kuchunguza maombi ya ulinzi wa kimataifa
- ✔ kusaidia kufuatilia uhamiaji halali na haramu katika nchi za EU+
- ✔ kushirikiana taarifa kati ya mamlaka za kitaifa na kuzuia uhalifu na ugaidi
- ✔ kuhakikisha kuwa watoto wanaowasili Ulaya wanaweza kufusaidiwa na kulindwa
- ✔ kuhakikisha hifadhidata nyingine za Ulaya zinazohusisha taarifa kuhusu masuala kama vile viza zinafanya kazi ipasavyo.



➤ NI DATA ZA WATU GANI ZINAZO HIFADHIWA KATIKA EURODAC

Eurodac ina data za watu ambao si raia wa nchi ya EU+ ambao:

- ✔ wameomba ulinzi wa kimataifa
- ✔ wamevuka mpaka wa nchi ya EU+ bila ruhusa
- ✔ Wameletwaa katika nchi ya EU+ baada ya kuokolewa kutoka baharini
- ✔ wanaishi kinyume na sheria katika nchi ya EU+
- ✔ wamewasili katika nchi ya EU+ kupitia mpango wa Umoja wa Ulaya wa kuwapatia makazi mapya au mpango wa kibinadamu wa kuwakaribisha wageni au mpango wa kitaifa wa kuwapatia makazi mapya
- ✔ wamepewa ulinzi wa muda mfupi.

➤ NANI ANAWEZA KUONA DATA ZANGU?

Mamlaka za kitaifa za hifadhi katika nchi ya EU+ zitachukua data zako za kibayometriki na kuzipeleka, pamoja na data nyingine muhimu, kwa Eurodac na kupokea matokeo ya kulinganisha.

Wakala wa Umoja wa Ulaya wa Ushirikiano wa Utekelezaji wa Sheria na polisi wa kitaifa wanaweza kuomba ufikiaji wa Eurodac kwa madhumuni ya kuzuia, kugundua na kuchunguza uhalifu mkali na ugaidi. Wanaweza kutafuta data zako katika Eurodac.

! MAMBO YA KUZINGATIA! Mamlaka wa nchi yako hawataweza kufikia taarifa hii.

➤ VITAKUWAJE NIKIKATAA KUTOA ALAMA ZA VIDOLE VYANGU?



Kwa mujibu wa sheria, unalazimika kutoa data yako ya kibayometriki.

Kuna sababu muhimu kwa nini alama zako za vidole zinahitajika. Ikiwa umeomba hifadhi, hii ni hatua muhimu katika utaratibu wa kuchunguza ombi lako.

Data ya alama za vidole inaweza pia kusaidia kupata wanafamilia waliopo katika nchi za EU+.

Ikiwa ncha za vidole vyako zimeharibika, alama za vidole zitachukuliwa tena baadaye.

Ikiwa utaharibu alama zako za vidole kwa makusudi, kutakuwa na matokeo hasi.

Kwa mfano, ikiwa umewasilisha ombi la hifadhi, taratibu zinaweza kusitishwa.

Ikiwa taratibu zitasitishwa kwa upande wako, hii inamaanisha kuwa hutachukuliwa tena kama mwombaji (mtafuta hifadhi). Utapoteza haki zote zinazohusiana na hadhi hiyo, sasa na siku zijazo.

Mamlaka za nchi za EU+ zinaweza kutumia nguvu kama njia ya mwisho ili kupata data yako ya kibayometriki. Pia zinaweza kukuzuia, kama hatua ya mwisho, ili kubaini au kuthibitisha utambulisho wako.

Ukataka kutoa data ya alama za vidole vyako kwa mamlaka katika nchi hii, kutakuwa na matokeo maalum.

Kukataa kutoa data ya alama za vidole kwa mamlaka katika nchi hii ni sababu ya Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa kuondoa ombi lako la ulinzi wa kimataifa bila kutaja.

NINA HAKI GANI KAHUSU DATA ZANGU KATIKA EURODAC?

Kila nchi ya EU+ ina mamlaka yanayodhibiti matumizi ya data. Una haki ya kuwasiliana na mdhibiti wa data na afisa wa ulinzi wa data na kuomba kupata data zako zilizohifadhiwa katika Eurodac.

Unaweza kuomba taarifa zako zirekebishwe ikiwa unahisi kuwa:

- haziko sahihi na zinahitaji kurekebishwa
- hazijakamilika na zinahitaji kusasishwa

Unaweza kuomba taarifa zako zifutwe ikiwa unahisi kuwa:

- zimeingizwa kwenye Eurodac kinyume na sheria.

Unaweza kupata maelezo ya mawasiliano ya mdhibiti wa data na afisa wa ulinzi wa data kwenye ukurasa wa mwisho wa brosha hii, wenye kichwa **'taarifa nyingine muhimu'**.

Ikiwa ungependa kutoa malalamiko rasmi kuhusu utunzaji wa data zako, unaweza kuwasiliana na mamlaka ya kitaifa ya usimamizi.

Unaweza kupata maelezo ya mawasiliano ya mamlaka ya kitaifa ya usimamizi kwenye ukurasa wa mwisho wa brosha hii.

TAARIFA NYINGINE MUHIMU

ITAARIFA KUHUSU MAELEZO YA MAWASILIANO YA MAMLAKA ZA KITAIFA ZA UDHIBITI WA DATA

Hapa chini unaweza kupata taarifa kuhusu jinsi ya kuwasiliana na ofisi ya udhibiti na afisa wa ulinzi wa data katika nchi hii.

Mdhibiti wa data anaweza kukujulisha ni data zipi zako za kibinafsi zimehifadhiwa katika Eurodac. Ikiwa data zako za kibinafsi hazijahifadhiwa kwa usahihi, unaweza kuomba data hizi zirekebishwe.

Ikiwa unahisi taarifa zako zozote zimetumiwa kinyume na sheria unaweza kuomba taarifa hizi zifutwe kwa kutumia maelezo ya mawasiliano yaliyo hapa chini.

Maelezo ya mawasiliano ya mdhibiti wa data ni: Ofisi ya Ulinzi wa Kimataifa, Uwasilishaji wa Huduma za Uhamiaji, 79-83 Lower Mount Street, Dublin 2, D02 ND99 au contact@ipo.gov.ie

TAARIFA KUHUSU HAKI ZA MLENGWA WA DATA

Katika nchi hii, una haki zifuatazo maalum kuhusiana na matumizi ya data zako binafsi..

Maelezo kuhusiana na haki zako za ulinzi wa data yanaweza kupatikana katika Idara ya Haki, Mambo ya Ndani na Sera ya Ulinzi wa Data ya Uhamiaji inayopatikana katika <https://assets.gov.ie/static/documents/department-of-justice-data-protection-policy.pdf> Unaweza kuwasiliana na Afisa wa Ulinzi wa Data wa Idara ya Haki, Mambo ya Ndani na Uhamiaji kwa barua pepe kwa: dataprotection.com

TAARIFA KUHUSU MAWASILIANO YA MAMLAKA YA KITAIFA ZA ULINZI WA DATA

naweza kutumia taarifa zifuatazo kuwasiliana na mamlaka ya kitaifa ya ulinzi wa data katika nchi hii..

Unaweza kutoa malalamiko rasmi kwa mamlaka ya kitaifa ya ulinzi wa data ikiwa unahisi kuwa data zako zozote za kibinafsi zimeshughulikiwa kinyume na sheria.

Maelezo ya mawasiliano ya Tume ya Ulinzi wa Data ni: 6 Pembroke Row, Dublin 2, D02 X963 au unaweza kuwasiliana nao mtandaoni katika <https://forms.dataprotection.ie/contact>



An Roinn Dlí agus Cirt,
Gnóthaí Baile agus Imirce
Department of Justice,
Home Affairs and Migration

Brosha hii itatumiwa kwa madhumuni ya taarifa pekee. Haileti haki wala wajibu wowote. Shirika la Umoja wa Ulaya la Hifadhi (EUAA) limetoa sehemu kuu ya nyenzo hii, na unakili na mabadiliko ya brosha hii yameruhusiwa na EUAA kwa Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya pekee. EUAA haikubali jukumu lolote au uwajibikaji wowote kwa usahihi, yaliyomo, ukamilifu, kisheria au uaminifu wa taarifa zilizojumuishwa katika brosha hii na Nchi Wanachama wa EU au na mtu mwingine yeyote anayehusika. Wala EUAA wala mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya EUAA hawawajibiki kwa matumizi yanayoweza kufanywa ya taarifa zilizomo katika brosha hii.

© Shirika la Umoja wa Ulaya la Hifadhi, 2025